TANGAZO LA SERIKALI NA 27 LA TAREHE 10/03/2006

SHERIA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI 1982)
(NA. 8 YA 1982)
SHERIA NDOGO
Zimetungwa chini ya kifungu cha 80.
SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI (USAFI WA MAZINGIRA) ZA MWAKA 2006

Jina na kuanza kutumika:

1 Sheria ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Manispaa ya Moshi (Usafi wa Mazingira) za mwaka 2006 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye gazeti la serikali.

Eneo la Kutumika:

2. Sheria ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Manispaa ya Moshi

Tafsiri:

3. Katika Sheria Ndogo hizi tafsiri za maneno zitatumika kama ifuatavyo:-

"ada ya kuondoa Taka" ina maana kiwango cha fedha kilichowekwa na Halmashauri kulipia gharama za kuzoa taka kama ilivyofafanuliwa na Sheria ndogo za Halmashauri ya Manispa ya Moshi (Ada na Ushuru) 2006;

"huduma" maana yake ni kusafisha, kuondoa, kukusanya na kutupa taka za viwandani, biashara na majumbani;

"chombo cha taka taka" ina maana ya pipa la taka lenye mfuniko chombo kingine chochote kilichokubaliwa na Halmashauri ambacho kimewekwana mwenye nyumba au mpangaji kwa ajili ya kuhifadhia taka taka kutoka kwenye jengo husika;

"chakula" ina maana ya kitu chochote kinachotumika kama chakula au kinywaji kwa binadamu isipokuwa vipodozi, dawa, tumbaku na pia inajumuisha;

(a) Kitu chochote kinachotumika kwa kutengeneza chakula
(b) Kitu chochote kinachowekwa kwenye chakula kama ladha.
(c) Rangi yoyote inayowekwa kwenye chakula

"eneo lililozuiwa" ni maeneo yote yaliyoko chini ya mamlaka ya Halmashauri ambapo majani marefu na mimea imepigwa marufuku kuwepo na inahusisha maeneo ya wazi, mitaa na barabara;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Moshi**;**

"Mkurugenzi" Maana yake ni Mkurugenzi wa Manispaa pamoja na anayekaimu;

"kuzuia" ni kitendo kinachofanywa na mtu kwa kukataza au kuashiria kukataza moja kwa moja na mtu ambaye amepewa mamlaka na Halmashauri kutekeleza sheria ndogo hizi aidha kwa kutumia nguvu au vitisho;

"Kaya" Maana yake ni familia ya baba, mama, watoto na wategemezi;

"Mzabuni" ina maana ya Mtu au Kikundi cha watu au Makampuni yaliyoidhinishwa na Halmashauri kufanya kazi zozote kama atakavyoekelezwa na Halmashauri;

"Mahakama'' maana yake ni mahakama ya ngazi yoyote na italihusisha pia baraza la Kata;

"majani" maana yake ni majani au vichaka vyenye urefu wa sm. 30 au zaidi vilivyopo maeneo yaliyokatazwa na pia inahusisha mazao yaliyopigwa marufuku kama ilivyotafsiriwa katika sheria ndogo za kilimo za Manispaa ya Moshi za mwaka 1984;

"maji taka" ina maana ya kinyesi au mkojo na uchafu mwingine kama matapishi, mate na maji machafu yanayotokana na uoshaji nguo, maji ya kuoga na maji ya kupigia deki, kuosha vyombo, maji yanayotokana na mvua kwenye mitaa, pia uoshaji wa magari, maji yanayotokana na uchafu kutoka vituo vya mafuta na viwandani ambayo yana kemikali au yasiyokuwa na kemikali na ambayo hayajasafishwa;

"mzigo wa Taka (Bundle waste) ni pamoja na pingili/sehemu za miti, matawi ya miti, vichaka vilivyofyekwa, magazeti, vijarida, masanduku ya karatasi au taka ngumu zilizofungwa kuwa mzigo uliofungwa vizuri na usiozidi mita moja kwa urefu au uzani wa kilo 15;

"Mtaa" inajumuisha barabara yoyote ndogo au kubwa au njia ya miguu au barabara nyembamba ya kufanya usafi au ya kwenda kwa miguu ipitayo kwenye maeneo ya wazi ambayo inatumika na jamii na pia inajumuisha daraja au kantara lipitalo juu ya barabara au njia;

"Mkazi/Mmiliki" inajumuisha mtu yeyote aliyetwaa na kumiliki eneo au nyumba ya kuishi au ya biashara bila kujali jina au cheo anachotumia kumiliki na kuwa mpangaji wa nyumba ya kulala hata kama amepanga chumba kimoja au hata kama wako wapangaji wengi;

"Mwenye nyumba" inamaanisha mwenye jina la milki na inajumuisha mtu yeyote mwenye jina kisheria la kumiliki nyumba au wakala wake au mtu yeyote anayepokea kodi ya pango kwa niaba yake;

"wakala" ina maana mzabuni aliyeteuliwa na Halmashauri kutoa huduma zinazohusiana na udhibiti wa taka ngumu au maji taka kwa niaba yake;

"taka" ina maana takataka zote zinazozalishwa majumbani, kwenye taasisi, maeneo ya biashara na viwandani pamoja na takataka zote zinazozalishwa mahali popote zisipostahili, mizoga, magari mabovu lakini haihusishi maji taka;

"makazi" ina maana nyumba, ghorofa au jengo lolote linalotumiwa kwa kuishi, pia inajumuisha ardhi ambayo haijaendelezwa lakini imetolewa kwa ajili ya nyumba za kuishi;

"nyumba" maana yake ni jengo la aina yoyote lililojengwa na linajumuisha nyumba za makazi;

"premises" inajumuisha ardhi, majengo, magari, mabehewa ya reli au vyombo vingine vya kubebea, mahema, mikokoteni, gari la mizigo, ujenzi wa aina yoyote, mifereji, maziwa ya bahari, ufuko, bomba la maji au eneo lolote liwe wazi au limefunikwa au liwe limeendelezwa au bado kisheria, pia meli, mashua/mtumbwi. Winch au chombo chochote cha majini/baharini kitakachokuwa kwenye bwawa/ziwa, mto, barabara au katika eneo lolote la Manispaa;

"rundo kubwa" (Bulk waste) ni pamoja na zana kubwa, mashine, samani na taka ngumu nyingine (lakini hazihusishi marundo ya vitu vya ujenzi au vitu vilivyobomolewa kwenye majumba, au wanyama waliokufa wenye uzito mkubwa zaidi ya uleuliobainishwa kwenye 'mzigo wa taka' (bundle waste);

"sewer" (Bomba la maji taka) ni mtandao wa mabomba kwa ajili ya kusafirisha maji taka kutoka katika nyumba au sehemu nyingine ya maji taka yanapozalishwa;

"soko" ina maana ya soko lililowekwa na halmashauri kisheria au eneo ambalo linatambulika kisheria na Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ya kufanyia shughuli za biashara;

"**taka ngumu"** ina maana taka taka zote zinazozalishwa majumbani, kwenye taasisi, maeneo
ya biashara na viwandani pamoja na takataka zote zilizofichama mahali popote zisipostahili, lakini haihusishi maji taka au taka miminika;

"taka za majumbani" (Domestic Refuse) ina maana taka za kawaida zilizozalishwa kwenye nyumba za kuishi;

"**taka za Biashara"** ni taka zote zile zitokazo kwenye maeneo ya biashara au viwandani kwa kuzalishwa na viwanda vyenyewe au wakati huduma zinapotolewa ambazo sio kwenye makazi ya watu na hujumuisha taka nyingine zote ambazo sio za majumbani;

"Taka hatari" ina maana taka zenye sumu, taka zinazoweza kuwaka moto, taka zinazoweza kula mwili au vyuma, taka zenye mionzi ya kuru nuturisha (radioactive), taka zinazoweza kulipuka au taka zilizo hatari kama ilivyobainishwa na taasisi ya kulinda mazingira ya Tanzania (Tanzania Environment Protection Agency) inajumuisha mafuta ya diesel, mafuta ya taa, petroli, rangi, mafuta ya kuyeyushia (solvent), betri za tochi, betri za magari, madawa ya kuulia wadudu waharibifu, na taka za hospitali au zinazoambukiza maradhi kutoka hospitali na zahanati, mafuta mazito ya kuteleza, pamoja na mafuta ya kulainisha na kuchanganya na vitu vingine kutoka kwenye viwanda, asbestos, madawa ya kuulia wadudu, taka za kugeuza umbile, mizoga au maiti;

"Upande wa mbele wa Nyumba" ina maana eneo lote la mbele ya nyumba na eneo lililoko kati ya nyumba na barabara inayopakana na nyumba hiyo au kuungana na eneo la nyumba pamoja na eneo la hifadhi ya barabara linalopitisha maji ya mvua hadi katikati ya barabara hiyo.

"kero" maana yake ni kitu chochote ambacho kimewekwa au kujengwa katika hali ya uchafu na kinaweza kusababisha:-

(a) madhara kwa maisha ya binadamu, wanyama au kiungo chake.
(b) chenye kuleta adha.
(c) kitu chochote kinachoweza kusababisha magonjwa.

Uwezo wa 4. (i) Afisa yeyote aliyeidhinishwa na Halmashauri atakuwa na uwezo wa kukagua

kuingia na kukagua:

eneo lolote lililopo chini ya Mamlaka ya Halmashauri kwa nia ya kuangalia chukizo na kutoa maelekezo ya kuondoa chukizo hilo.

(ii) Maafisa hao ni Mkurugenzi pamoja na watendaji wake na inajumuisha pia wenyeviti na watendaji wa Mitaa na Kata

Kuweka taka katika mitaa na maeneo:

5. (1) Ni marufuku mtu yeyote kuweka au kutupa taka, mchanga au uchafu wowote eneo lolote lililokatazwa na Halmashauri
(2) Itakuwa ni kosa kukiuka au kwenda kinyume na kifungu cha 5(1) cha Sheria Ndogo hizi.

Kukusanya na kuhifadhi taka:

6. (1) Mtu yeyote anayemiliki nyumba au mpangaji wa nyumba anatakiwa kuweka chombo cha kukusanya taka chenye ukubwa unaotosheleza na kiwe na mfuniko unaofaa na kinatakiwa kitumike kila siku katika nyumba hiyo.
(2) Ukusanyaji wa taka ngumu utafanywa na Halmashauri au mtu yeyote aliyeidhinishwa na Halmashauri kufanya kazi hiyo kwa niaba ya Halmashauri na ada ya uzoaji taka inatozwa kulingana na Sheria Ndogo za ushuru na ada za mwaka 2006.
(3) Kulingana na vifungu vidogo 1 na 2 cha kifungu na 6, ni marufuku kwa mtu yeyote kuweka katika chombo cha kuhifadhia taka au maji machafu kitu chochote ambacho kinaweza kuleta madhara kwa binadamu au kusababisha moto.
(4) Takataka zote zihifadhiwe ndani ya ua mpaka hapo zitakapochukuliwa na Halmashauri au mwenye nyumba au mpangaji kuzipeleka mwenyewe kwenye maeneo maalumu yaliyotengwa.

Vifaa vya Kuhifadhia tatakata:

7. Mmiliki wa nyumba au mpangaji wa nyumba atalazimika kutunza takataka zilizohifadhiwa kwenye pipa la taka au chombo chochote kinachokubalika kisheria hadi hapo Halmashauri au mtu yeyote aliyeteuliwa na Halmashauri kuzichukua na kuzitupa jalalani.

Uwekaji wa vyombo vya kuhifadhia taka:

8. (1) Ni jukumu la mwenye nyumba au mpangaji kuweka chombo cha kuhifadhia taka katika nyumba yake na kuwezesha ukusanyaji wa taka hizo kwa urahisi
(2) Kila mwenye basi litakaloingia eneo la Manispaa atawajibika kuwa na chombo cha kuhifadhi taka na kuhakikisha kwamba kila abiria anatupa taka humo.
(3) Itakuwa ni kosa kwa mwenye basi au dereva au kondakta iwapo abiria aliyeko ndani ya basi lake atatupa kitu chochote barabarani au stendi.
(4) Mwenye basi au dereva au kondakta atawajibika kulipa faini ya shilingi elfu thelathini baada ya kujaziwa fomu ya ilani na afisa wa Manispaa.

Utupaji au uchomaji wa taka:

9. Ni marufuku kwa mtu yeyote kumwaga takataka au kuzichoma moto ovyo bila idhini ya Halmashauri.

Ukataji wa majani:

10. Mwenye nyumba au mpangaji anatakiwa kukata majani yasizidi kimo cha sm 15 na kukata uzio na kuondoa mabaki na kuyaweka kwenye chombo cha kuhifadhia taka au sehemu iliyoruhusiwa kuhifadhi taka hizo.

Utupaji wa taka:

11. Ni marufuku mtu yeyote kumwaga, kutiririsha maji taka katika mtaa, uchochoro, eneo la wazi, mtaro ulio wazi au mashimo yasiyoruhusiwa.

Matumizi ya mashimo ya maji taka:

12. Utakuwa ni wajibu wa mwenye nyumba kuunganisha choo cha maji na uchafu wake kwenye mtaro wa maji taka, iwapo atsshindwa kufanya hivyo atatakiwa aelekeze uchafu huo katika mashimo ya maji taka yaliyokubaliwa na Halmashauri.

Uchafuzi wa maji:

13. (1) Ni marufuku mtu yeyote kuchafua au kuvuruga maji yanayotumika na binadamu au mnyama.
(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuoga au kufulia kwenye chanzo cha maji, mto au mfereji au tangi ambalo halikuwekwa kwa madhumuni hayo.

Mwenye nyumba/mpangaji kuondoa kero:

14. Endapo kutatokea chukizo lililosababishwa na maji taka katika nyumba yenye mpangaji
zaidi ya mmoja na iwapo mwenye nyumba hawezi kupatikana kwa haraka, Halmashauri inaweza kuamuru wapangaji kufanya lolote linalowezekana ili kuondoa chukizo na gharama hizo zitafidiwa na kodi watakayomlipa mwenye nyumba.

Vyoo:

15. (1) Endapo Halmashauri itagundua kwamba nyumba inayokaliwa na watu vyoo vyake viko katika hali ya uchafu au hatari kwa afya ya binadamu. Halmashuauri itatoa notisi kwa mwenye nyumba au mpangaji kutengeneza vyoo hivyo kwa kiwango kinachoridhisha kwa mujibu wa maelezo yaliyopo katika notisi hiyo.
(2) Mtu yeyote anayemiliki jengo au nyumba inayotumika kama makazi anatakiwa aweke vyoo vya kutosha kama Halmashauri itakavyoona inafaa.
(3) Mtu yeyote anayemiliki kiwanda, shule, mgahawa, shule za bweni, hotel au jengo lolote la umma, sehemu za burudani, au nyumba yoyote atatakiwa kuweka vyoo vinavyoridhisha kwa ajili ya matumizi ya wanaume na wanawake na atahakikisha vyoo hivyo vina maji, mwanga na hewa ya kutosha.
(4) Ni marufuku mtu yeyote kuendesha biashara ya nyumba ya wageni au hostel ya wanafunzi bila ya kibali cha Halmashauri.
(5) Kibali cha Hosteli ya wanafunzi au nyumba ya wageni kitatolewa kwa kuzingatia yafuatayo:-
    (a) Mwanga na hewa ya kutosha;
    (b) Nafasi;
    (c) Vifaa (samani) vya kutosha;
    (d) Uimara wa jengo;
    (e) Uondoshaji wa maji taka, taka miminika na taka ngumu.
    (f) Usafi wa jumla wa majengo na vifa vyake.
    (g) Utoshelezaji wa vyoo/bafu kwa jinsia zote.
(6) Kila mgahawa wa vyakula au vinywaji ni lazima uwe na vyoo vya kutosha kwa ajili ya wateja, watumishi na wapita njia.
(7) Hairuhusiwi kufunga milango ya vyoo kwa kufuli la aina yoyote ile.
(8) Atakayepatikana kafunga mlango wa choo kwa kufuli ili kuzuia wapita njia wasitumie vyoo atawajibika kulipa faini isiyopungua Tshs.30,000/= papo kwa papo.

Marufuku kutumia choo:

16. Choo cha aina yoyote ambacho kwa maoni ya Halmashauri kitaonekana kichafu au kuhatarisha maisha ya binadamu hakitaruhusiwa kutumika mpaka hapo Halmashauri itakaporidhika na matengenezo yaliyofanyika.

Uchimbaji wa

17. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba au kujenga shimo kwa ajili ya kuhifadhi

mashimo kwa ajili ya kuhifadhia kinyesi au maji taka:

kinyesi au maji taka bila idhini ya maandishi iliyotolewa na Halmashauri.

Utupaji wa kinyesi:

18. Ni marufuku kwa mtu yeyote kutupa kinyesi, mkojo, mate au matapishi katika uchochoro, mtaani au eneo lolote lisiloruhusiwa.

Utupaji wa maji taka ya viwanda:

19. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuendesha kiwanda chochote kinachotoa maji taka bila ya kuwa na mitambo ya kusafishia maji taka hayo ambayo imeidhinishwa na Halmashauri.
(2) Kwa maana hiyo ni marufuku mtu yeyote kuruhusu maji taka kutoka viwandani, au eneo lolote linalofanya utengenezaji kuingia katika vyanzo vya maji safi, ardhi, maeneo wazi, mitambo ya maji taka, uchochoro, mitaro iliyo wazi kabla ya kuyasalimisha kwa kiwango kinachokubalika na Halmashauri.
(3) Kila baada ya miezi mitatu kabla na baada ya kuyasafisha maji taka kutoka viwandani yatatakiwa kupimwa kuangaliwa ubora wake na maabara ya Serikali au maabara yoyote iliyoruhusiwa na Serikali na majibu au matokeo ya uchunguzi huo kuletwa Halmashauri.

Usafi eneo la nyumba:

20. (1) Ni marufuku mtu yeyote kusababisha au kuruhusu eneo la nyumba anayoishi kuwepo uchafu wa takataka au majani yoyote marefu.
(2) Itakuwa ni wajibu wa mmiliki/mpangaji wa nyumba kufagia na kuondoa uchafu au malundo ya uchafu na kuweka safi eneo la mbele la nyumba yake.
(3) Itakuwa ni wajibu wa mwenye nyumba kutunza sehemu ya nyuma ya nyumba yake kwa kutotupa taka pia kuondoa taka na nyasi ndefu.
(4)Vichochoro vyote vitatunzwa na wenye nyumba husika na kila mwenye nyumba/mpangaji atawajibika kutunza eneo linaloangukia kwake yaani kila nyumba itakuwa na kijisehemu katika uchochoro huo kwa mujibu wa Sheria.

Ni marufuku kutelekeza magari mabovu:

21. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutelekeza magari mabovu kwenye njia ya mguu, mtaa au vichochoro au mitaro iliyo wazi na kusababisha adha kwa wakazi au watumiaji wa njia hiyo.
(2) Ni marufuku mtu yeyote kutengeneza gari au mtambo eneo ambalo sio mahususi kwa shughuli hiyo au eneo lisiloruhusiwa na Halmashauri.
(3) Ni marufuku mtu yeyote kuosha magari au mitambo ya aina yyote ile katika eneo lisiloruhusiwa na Halmashauri.

Halmashauri au wakala kukusanya na kutupa taka ngumu:

22. (1) Halmashauri au mtu yeyote aliyeteuliwa kama Wakala atakuwa na uwezo wa kukusanya, kuhifadhi, kusafirisha na kutupa taka za majumbani na biashara kwa kulipia kama ilivyoainishwa katika Sheria Ndogo ya ada na ushuru ya mwaka 2006.
(2) Kamati za maendeleo za Mitaa na Kata zitakuwa na uwezo chini ya sheria hii kusimamia usafi kwenye maeneo yao kwa kukomesha utupaji taka ovyo na usafishaji wa vichochoro.
(3) Kamati za Maendeleo za Mitaa na Kata zitakuwa na uwezo wa kumtoza yeyote atakayechafua mazingira kwa namna yoyote ile faini isiyozidi shs. Elfu kumi.
(4) Iwapo mchafuzi wa mazingira hatakuwa na fedha ya kulipa pindi anapokamatwa Kamati husika itawajibika kukamata mali yake yenye thamani kama hiyo fedha.

(5)Kama hana fedha wala mali apewe adhabu ya kusafisha kwa kadiri mamlaka/mtaa/kata itakavyoona inafaa.
(6) Fedha zitakazopatikana kwa njia hii zitatumika kwenye shughuli za maendeleo za Mtaa au Kata husika na ni lazima zikatiwe stakabadhi rasmi ya Mtaa au Kata husika.
(7) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kumzuia mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Mtaa au Kata kutimiza matakwa ya sheria.

Taka za Nyumbani:

23. Kila mkazi kwenye nyumba au mpangaji kwenye nyumba ya makazi atawajibika kuweka chombo cha kuridhisha cha kuweka taka za majumbani chenye ujazo unaoridhisha na chenye mfuniko unaofaa na kuhakikisha kuwa takataka zote zinazozalishwa kwenye nyumba hiyo zinawekwa humo kila siku, mradi chombo hicho kiwe kinatosheleza kuweka taka zote. Takataka hizo zitatolewa nje pindi gari la kuzisomba linapopita au kupelekwa kwenye ghuba za taka zilizopo mitaani.

Taka za Biashara:

24. (1) Kila mkazi kwenye nyumba ya biashara au mpangaji atalazimika kuweka chombo cha kuridhisha cha kuhifadhi taka za biashara chenye ujazo wa kuridhisha na mfuniko wa kubana na kuhakikisha kuwa taka zote zinazozalishwa zinahifadhiwa kwenye chombo hicho na ujazo wake utosheleze kwa siku.
(2) Halmashauri kama itakavyoona inafaa itaelekeza sifa za chombo hicho na ujazo wake utosheleze kwa siku
(3) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kukiuka matakwa ya kifungu kidogo cha 24(1) na atiwapo hatiani atawajibika kulipa faini ya shs. elfu hamsini au kwenda gerezani kwa kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja, faini na kifungo.

Ujenzi au kukarabati nyumba:

25. (1) Hairuhusiwi mtu au kikundi cha watu kubomoa jengo lolote kwa nia yoyote ile bila kupata kibali cha Halmashauri kwanza.
(2) Kila anayetaka kubomoa nyumba atatakiwa kuomba kibali cha kubomoa nyumba na kutoa malipo ya awali kabla ya kubomoa. Malipo hayo ni kwa ajili ya gharama za kuondoa vifusi na mabaki ya kubomoa kwa kadri itakavyokuwa imetathminiwa na Halmashauri.
(3) Mtu yeyote anayetaka kujenga au kukarabati jengo lolote atatakiwa kuhifadhi vifusi na vifaa vingine vya ujenzi ndani ya eneo au kiwanja chake na sio barabarani au kwenye hifadhi ya barabara.

Taka hatari na viwango vya malipo vya ukusanyaji na utupaji:

26. (1)Kila mwenye nyumba na mtumiaji wa sehemu ambapo taka za viwandani zinazalishwa kwa malundo au taka za hospitali au taka zozote zinapozalishwa atapaswa kuzitunza taka hizo na kuhakikisha kuwa anaziondoa kwa usanifu wa kuridhisha au jinsi atakavyoelekezwa mara kwa mara na Halmashauri.
(2)Halmashauri itatoza ada za uzoaji taka kwa biashara zote kulingana na ukubwa wa uzalishaji, kwenye makazi, taka hatari na maeneo mengine kama Halmashauri itakavyoona inafaa.
(3)Mtu yeyote atakayevunja sheria hii ndogo atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atapewa adhabu ya faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo cha miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja kifungo na faini, vilevile atatakiwa kurejesha gharama za uharibifu atakaokuwa amesababisha.
(4)Itakuwa ni kosa mtu yeyote kuweka mtambo au mashine au gari, pikipiki n.k. inayochafua hewa kwa kutoa Moshi mzito au mwingi unaosababishwa na

uchakavu wa chombo chenyewe.

Mahali pakuweka taka:

27 (1)Kila mmiliki/mkazi wa nyumba ya makazi au nyumba ya biashara atawajibika kuweka taka zote azalishazo mahali atakapoelekezwa na Halmashauri. Iwapo mtu yeyote atashindwa kufanya hivyo atakuwa ametenda kosa.
(2)Mtu yeyote atakayevunja Sheria Ndogo hii, atakuwa ametenda kosa na akithibitika kuwa ametenda kosa atapigwa faini isiyopungua shilingi elfu thelathini (30,000/=) na isiyozidi elfu hamsini (50,000) au kifungo cha miezi kumi na mbili au vyote kifungo pamoja na faini.

Utaratibu wa kukusanya taka:

28 (1) Halmashauri itaweka mipango na utaratibu wa ukusanyaji na utupaji taka kutoka kwenye sehemu za biashara na nyumba za kuishi na kuzizoa taka hizo na kuzitupa.
(2) Halmashauri inaweza kufanya kazi ya kukusanya taka yenyewe au kuteuwa Wakala kwa makubaliano maalum.

Ufungaji mazao au vitu vinavyoharibika kwa kosa:

29. (1)Mzalishaji yoyote, mfanya biashara au mchuuzi wa mazao au vitu vinavyoharibika au mtu yeyote anayejishughulisha na mazao au vitu vinavyoharibika au kuoza kwa haraka haruhusiwi kuingiza sokoni vitu hivyo vikiwa vimefungwa au kufunikwa kwa majani, majani ya miti au aina nyingine yoyote ya sehemu ya mmea.
(2)Itakuwa halali kwa Mkurugenzi au mtu mwingine aliyeidhinishwa kuelekeza aina ya chombo kitakachopendekezwa kutumika kupakia mazao au vitu vinavyoweza kuharibika iwapo mazao hayo yatatakiwa kuletwa ndani ya eneo la Halmashauri ya Manispaaa ya Moshi. Kila mzalishaji, mfanyabiashara au mchuuzi atalazimika kufuata maelezo hayo.
(3) Halmashauri kadri itakavyoona inafaa inaweza kusitisha uingizaji au kulazimisha kutolewa, kutoka kwenye masoko aina yoyote ya mazao au vitu vinavyoharibika ambavyo hufungwa na kupakiwa kama ilivyo kwenye vifungu vidogo 29 (1) cha Sheria Ndogo hii.

Ufugaji mjini

30. (1)Kila mfugaji wa ng'ombe, mbuzi, kuku nguruwe na wanyama wengine wa nyumbani atawajibika kukusanya na kuhifadhi uchafu wowote utokanao na wanyama hao kama vile kinyesi, manyoya, utumbo, baada ya kuchinjwa na uchafu utokanao na ufugaji huo mfano nyasi au mabaki ya vyakula vyao katika hali ambayo itaridhisha Halmashauri na ambayo haitaleta kero kwa jamii.
(2) Kila atakayetaka kufuga wanyama waliotajwa kweye kifungu kidogo cha 30(1) ni budi awe na eneo la kutosha.
(3) Hairuhususiwi kabisa kufuga aina yoyote ya wanyama wanaotajwa kwenye kifungu kidogo cha 30 (1) kwenye eneo la msongamano wa makaazi.
(4) Kwa namna yeyote ile ufugaji ni lazima uwe wa mnyama kuwa pahala pamoja na sio kuzurura ovyo.

Kudai madeni:

31. Ada yoyote ya kuzoa taka inavyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi itakuwa ni deni kwa Halmashauri au wakala wake na inaweza kudaiwa kutoka kwenye kaya au mmiliki kwa mujibu wa sheria.

Jinsi ya Utekelezaji:

32. (1)Madeni ya ada ya kuondoa taka ilioainishwa kwenye kifungu cha 31 yatakusanywa kutoka kwa mmiliki kwa kumpelekea Hati ya Madai kwa

maandishi na iwapo atashindwa kulipa kwa muda wa siku 14 Halmashauri au mtu yeyote aliyeidhinishwa anaweza kufungua kesi ya madai Mahakamani au kukamata mali ya mdaiwa yenye thamani ya kiasi anachodaiwa.

(2)Mali iliyokamatwa kwa jinsi hii itauzwa kwa mnada wa hadhara iwapo mhusika hata ikomboa ndani siku ishirini na moja (21) tangu siku ilipokamatwa.

(3)Baada ya uthibitisho wa Mkurugenzi au Afisa aliyeidhinishwa juu ya deni lenyewe na kuhakikisha kuwa mmiliki hajalipa licha ya kupelekewa madai, Mahakama itathibitisha madai hayo na hivyo itakuwa hati ya idhini ya kutekeleza hukumu dhidi ya madai hayo kwa njia yoyote ile na itakuwa sawa na idhini ya kukamata mali na idhini ya kuuza mali iliyokamatwa sawa na inayotolewa na mahakama hiyo kwenye kesi nyingine za madai.

Uthibitisho:

33. Kila shahada inayopelekwa katika mahakama, kama ilivyo kwenye kifungu cha 32 hapo juu itakuwa ni kielelezo cha kweli cha kuonyesha maelezo yaliyotolewa na sahihi.

Utoaji wa leseni:

34. (1)Isipokuwa pale ambapo sheria andishi nyingine inaeleza vinginevyo, Mkurugenzi anaweza kufuta leseni ya biashara pale ambapo mmliki au mwenye biashara atakaposhindwa kuonesha stakabadhi ya kulipia ada ya taka.

(2)Kabla ya kufuta leseni hiyo, Halmashauri au Afisa aliyeruhusiwa atatakiwa atoe ilani ya maandishi ya siku zisizopungua kumi na nne kueleza nia ya kufanya hivyo kwa kumtaka mhusika alipe Ada hiyo mara moja.

Muda wa kulipa ada:

35. Ada itatakiwa kulipwa siku thelathini baada ya Mmiliki, mpangaji au mfanyabiashara kupata taarifa.

Wakala:

36. Halmashauri inaweza kumteua mtu yeyote kukusanya ada na au kuzoa taka na inaweza kuingia naye Mkataba wa kufanya kazi za ukusanyaji na uzoaji taka ikiwa ni pamoja na kumpa uwezo wa kumpeleka mahakamani mtu yeyote anayeshindwa kulipa ada ya ukusanyaji au uzoajiau taka kwa mujibu wa sheria ndogo.

Kuzuia kero:

37. (1) Iwapo kero itaonekana mahali pa au karibu na makazi kwa sababu ya biashara au taka za majumbani kutupwa eneo la makazi, Halmashauri itampa ilani mmiliki au mkazi anayeishi kwenye nyumba hiyo na kumtaka aondoe kero hiyo kwa muda utakaotakiwa kwa maandishi na iwapo muda aliopewa katika ilani utamalizika, kero ikawa inaendelea au kurudiwa atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi.

(2) Halmashauri inaweza kumtaka mmiliki au mkazi wa nyumba yoyote au mkazi kwenye nyumba ya makazi kuondoa kinyesi cha binadamu katika eneo lake.

Viwanja visivyokuwa na mtu:

38. Itakuwa ni kosa kwa Mtu yeyote au mmiliki wa kiwanja chochote au sehemu ya kiwanja ambacho hakikuendelezwa au kuwa na mtu au mwenye kiwanja au ambacho hakina mkazi kutupa mahali hapo kitu chochote kinachoudhi au kutupwa kwenye barabara au eneo lililo wazi kutoka nyumba yoyote ile iwe ni masalia ya vyombo vya vyakula makombo au masalia ya vyakula vya mifugo au kinyesi.

Wajibu wa

39. (1) Kila mwenye nyumba ya makazi au nyumba ya biashara atawajibika

kuwakilisha:

kumwakilisha mmiliki chini ya Sheria Ndogo hizi kwa makosa atakayofanya mmiliki au mpangaji wa nyumba hiyo ya makazi au ya biashara.

(2) Afisa yeyote au Wakala wa mamlaka ambaye ameidhinishwa na mamlaka hiyo kuiwakilisha anaweza kwa wakati anaoona inafaa kufanya ukaguzi,uchunguzi au kukagua utekelezaji wa kazi katika eneo lolote lililopo chini ya Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Ada ya utupaji taka kwenye dampo:

40. (1) Kutakuwepo na ada ya kutupa taka katika jalala kwa kila wakala, taasisi za jamii, taasisi zisizo za kiserikali na taasisi nyingine zozote ambazo zitajishughulisha kuzoa na kutupa taka kadri itakavyopangwa na Halmashauri.

(2) Taasisi zisizo za kiserikali na mtu yeyote atakayejishughulisha na uzoaji na utupaji taka ambaye atashindwa au kukataa kulipa ada ya utupaji taka atakuwa ametenda kosa na atatakiwa kulipa asilimia ishirini 20% zaidi ya ada kama adhabu.

Kosana adhabu:

41. (1)Mtu yeyote atakayekataa au atakayedharau au kushindwa kutekeleza Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na itakapothibitika atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini au kifungo cha miezi kumi na mbili au vyote viwili faini na kifungo kwa pamoja.

(2)Halmashauri itakuwa na uwezo kumtoza mvunjaji wa Sheria Ndogo hizi faini ya papo kwa papo kiasi kisichozidi shilingi elfu hamsini endapo mkosaji au mvunjaji atakiri kosa kwa kujaza fomu maalumu ambayo ni kiambatanisho kwenye Sheria Ndogo hizi.

(3)Mtuhumiwa atakuwa na haki ya kukataa kosa na kwenda kujibu shitaka mahakamani kwa kujaza sehemu ya pili ya fomu hiyo na endapo mahakama itamtia hatiani atalipa gharama zote za kuendesha shauri tangu atende kosa, na kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini au kwenda gerezani miezi kumi na mbili au vyote faini na kifungo.

(4) Baada ya kumaliza adhabu aliyopewa na Kifungu cha 41(2) na (3) cha Sheria Ndogo hii mkosaji atawajibika kusafisha, kufanya marekebisho ya uharibifu aliofanya kadiri Halmashauri itakavyoona inafaa.

Jukumu la CBO's:

42. Kutakuwepo na CBO's zitakazokuwa zinafanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa Mji katika mitaa au Kata zao. CBO's zitawajibika kukusanya taka ngumu na kuzipeleka kwenye jaa pia zitawajibika kukusanya ada za taka ngumu katika maeneo wanayotoa huduma.

Wajibu wa Kamati za maendeleo za Mitaa/Kata:

43. (1)Kamati za maendeleo za Kata zikisaidiwa na zile za mitaa zitahusika katika utekelezaji wa shughuli zote za usafi pamoja na kulinda maslahi ya CBO's na Halmashauri.

(2)CBO's zitawajibika kuingia mkataba na Halmashauri wa kuendesha aina ya shughuli ya usafi wa Mji au kudhibiti taka ngumu kama watakavyoelekezwa na Halmashauri

Jukumu la Halmashauri:

44. Halmashauri itawajibika kuhamasisha uundaji wa CBO's kuzitambua, kuzipa nguvu za kisheria na kuziwezesha kuanza kazi.

Kufutwa kwa Sheria Tangazo la Serikali

45. Sheria Ndogo za Halmashauri ya Manispaa ya Moshi (usafi wa mazingira) za mwaka 2001 zinafutwa.

G.N.172/2001:

Nembo na Mhuri wa Halmashauri Manispaa ya Moshi umeshabandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuata Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika mnamo tarehe 28 mwezi April, 2005 na kushuhudiwa na:-

LUCAS TARIMO
Mstahiki meya
Halmashauri ya Manispaa ya Moshi

JOEL M. SHIMBA
Mkurugenzi wa Manispaa
Manispaa ya Moshi.

NAKUBALI

BRIG.JEN.(MST) HASSAN A.H.NGWILIZI (MB)
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na
Serikali za mitaa